Food and Agriculture Organization of the United Nations

Mwongozo wa Hiari wa Kuhakikisha Uvuvi Mdogo Unakuwa Endelevu

Kwa Muktadha wa Uhakika wa Chakula na Kuondoa Umaskini

Mwongozo wa Hiari wa Kuhakikisha Uvuvi Mdogo Unakuwa Endelevu

Kwa Muktadha wa Uhakika wa Chakula
na Kuondoa Umaskini

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo
Rome, 2018

The designations employed and the presentation of material in this information product do not imply the expression of any opinion whatsoever on the part of the Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO) concerning the legal or development status of any country, territory, city or area or of its authorities, or concerning the delimitation of its frontiers or boundaries. The mention of specific companies or products of manufacturers, whether or not these have been patented, does not imply that these have been endorsed or recommended by FAO in preference to others of a similar nature that are not mentioned.

The views expressed in this information product are those of the author(s) and do not necessarily reflect the views or policies of FAO.

© FAO, 2015 (English version)
© FAO, 2019 (Swahili version)

Some rights reserved. This work is made available under the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 3.0 IGO licence (CC BY-NC-SA 3.0 IGO; https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/3.0/igo/legalcode/legalcode).

Under the terms of this licence, this work may be copied, redistributed and adapted for non-commercial purposes, provided that the work is appropriately cited. In any use of this work, there should be no suggestion that FAO endorses any specific organization, products or services. The use of the FAO logo is not permitted. If the work is adapted, then it must be licensed under the same or equivalent Creative Commons license. If a translation of this work is created, it must include the following disclaimer along with the required citation: "This translation was not created by the Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO). FAO is not responsible for the content or accuracy of this translation. The original [Language] edition shall be the authoritative edition."

Disputes arising under the licence that cannot be settled amicably will be resolved by mediation and arbitration as described in Article 8 of the licence except as otherwise provided herein. The applicable mediation rules will be the mediation rules of the World Intellectual Property Organization http://www.wipo.int/amc/en/mediation/rules and any arbitration will be conducted in accordance with the Arbitration Rules of the United Nations Commission on International Trade Law (UNCITRAL).

Third-party materials. Users wishing to reuse material from this work that is attributed to a third party, such as tables, figures or images, are responsible for determining whether permission is needed for that reuse and for obtaining permission from the copyright holder. The risk of claims resulting from infringement of any third-party-owned component in the work rests solely with the user.

Sales, rights and licensing. FAO information products are available on the FAO website (www.fao.org/publications) and can be purchased through publications-sales@fao.org. Requests for commercial use should be submitted via: www.fao.org/contact-us/licence-request. Queries regarding rights and licensing should be submitted to: copyright@fao.org.

Kumbukumbu

Kwa heshima ya Chandrika Sharma, aliyekuwa Katibu Mtendaji wa International Collective in Support of Fishworkers (ICSF), mwanamama jasiri aliyejitolea kufanya kazi bila kuchoka ili kuboresha maisha ya jamii ya wavuvi wadogo duniani kote, na ambae alitoa mchango mkubwa katika maandalizi ya Mwongozo huu, kabla ya kupotea katika mkasa wa ndege ya shirika la ndege la Malaysia (MH 370) Machi, 2014.

Tafsiri ya Kiswahili

Hii ni tafsiri ya Kiswahili ya Kijitabu kilichoandaliwa na kuchapishwa mwaka 2015, na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Kilimo na Chakula (FAO), ambacho kwa lugha ya Kiingereza kinajulikana kama “Voluntary Guidelines for securing Sustainable Small-Scale Fisheries: in the context of food security and poverty eradication”.

Kutokana na umuhimu wa Mwongozo huu katika kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Kilimo na Chakula (FAO), imeona kuna umuhimu mkubwa wa kuandaa tafsiri ya Kiswahili, ili wavuvi wadogo na wadau wengine nchini na katika nchi za jirani, waweze kunufaika na yaliyomo. Hata hivyo, inapaswa kueleweka kwamba, lengo kubwa halikuwa kutafsiri neno kwa neno isipokuwa kuwasilisha maudhui makuu ya Mwongozo katika lugha ya Kiswahili.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi
Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Tanzania
P.O.Box 2847,
40487 **Dodoma**
Tanzania
Simu: +255 026 2963725
Fax: +255 026 2322613
E-Mail: ps@mifugouvuvi.go.tz
Web: http://www.mifugouvuvi.go.tz

Food and Agricultur Organization of the United Nations

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO)
Viale delle Terme di Caracalla
00153 **Rome**
Italy
Simu: + 39 0657051
Fax: +39 0657053152
Website: www.fao.org

Yaliyomo

Tafsiri ya Kiswahili v
Shukrani ix

Utangulizi

1. Mwongozo wa hiari; ni nini hasa? 2
2. Maudhui ya Mwongozo wa Hiari 3
3. Takwimu za ujumla za uvuvi mdogo 4
4. Umuhimu wa Mwongozo huu 4
5. Historia ya uandaaji wa Mwongozo 5
6. Maeneo Makuu na Mpangilio wa Mwongozo 6

Sehemu ya Kwanza:Utangulizi

7. Malengo mahususi 9
8. Chimbuko na wigo 9
9. Misingi Mikuu 9
10. Uhusiano na miongozo mingine 10

Sehemu ya Pili: Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi Mdogo

11. Kuwajibika Katika Usimamizi na Umiliki wa Maeneo 13
12. Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Uvuvi 14
13. Maendeleo ya Jamii, Ajira na Usalama kazini 14
14. Mnyororo wa Thamani, Uhifadhi na Biashara 15
15. Usawa wa Jinsia 16
16. Hatari za Majanga na Mabadiliko ya Tabia Nchi 16
17. Sehemu ya Tatu: Kujenga Mazingira Bora na Kusaidia Utekelezaji wa Mwongozo 16
18. Kuimarisha uhusiano na mashirikiano ya kisera baina ya taasisi mbalimbali 16
19. Kufanya Tafiti na Upashanaji wa Taarifa za Usimamizi wa Raslimali ya Uvuvi 17
20. Kujenga Uwezo wa Wadau na Taasisi 18
21. Kusaidia utekelezaji, ushirikiano na ufuatiliaji 18

Shukrani

Serikali inatambua mchango mkubwa uliotolewa na Mabwana Ali Thani na Baraka Kalangahe wa Mwambao Coastal Community Network, Tanzania na Dkt. Rosemarie Mwaipopo wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam kwa jitihada zao za awali walizofanya katika kutoa muhtasari wa tafsiri ya Kiswahili ya mwongozo. Muhtasari huo, uliochapwa kwa msaada wa International Collective in Support of Fishworkers (ICSF), umesaidia sana katika kuandaa tafsiri hii.

Shukrani zapekee nikwa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Kilimo na Chakula (FAO), kwa kuongoza mchakato wa uandaaji wa Mwongozo huu muhimu kwa mustakabali wa uvuvi mdogo hasa katika nchi zetu zinazoendelea. Mchango uliotolewa, na ambao unaendelea kutolewa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, ikiwa ni pamoja na International Collective in Support of Fishworkers (ICSF) Mwambao na EMEDO katika kuchagiza kutumika kwa Mwongozo huu, utaendelea kuthaminiwa.

Aidha, Mabwana Frances Wild na Ella Khafaji wamesaidia sana katika kuchora picha nyingi zilizotumika katika kijitabu hiki cha tafsri ya Mwongozo.

Utangulizi

Mwongozo wa hiari wa kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu; katika muktadha wa uhakika wa chakula na kuondoa umaskini umeandaliwa kama nyongeza ya Taratibu za Kimaadili za Uvuvi zinazozingatia uwajibikaji, ambazo ziliandaliwa chini ya uratibu wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) mwaka 1995 (Code of Conduct for Responsible Fisheries CCFRF) na kukubaliwa nchi nyingi duniani.

Aidha, Mwongozo huu wa hiari ni mahsusi kwa ajili ya kuangaza na kuweka taratibu zinazuhusu uvuvi mdogo. Sababu kuu iliyopelekea kuandaa Mwongozo maalumu kwa ajili ya uvuvi mdogo ni kwamba; kwa kiwango kikubwa jamii ya wavuvi wadogo imeendelea kuachwa nyuma, na umaskini katika jamii hizi umekuwa ni wa kiwango kikubwa. Hali hii ya kusikitisha inatokea wakati ambapo uvuvi mdogo huchangia nusu ya samaki wote wanaovuliwa duniani, na huajiri asilimia 90 ya wavuvi na wafanyakazi wengine katika Sekta ya Uvuvi duniani.

Hivyo, imeonekana kuna umuhimu mkubwa wa kuandaa Mwongozo huu, ili kuangazia changamoto mbalimbali zinazowakabili wavuvi wadogo, na kubainisha mbinu ambazo zinaweza kutumiwa katika kutatua changamoto hizo. Mwongozo unabainisha masuala yote muhimu katika mfumo mzima wa mnyororo wa thamani ikiwa ni pamoja na usimamizi wa rasilimali ya uvuvi, masuala ya maendeleo ya jamii ya wavuvi wadogo, thamani ya mazao na biashara, pamoja na umuhimu wa kujenga mazingira bora yanayoimarisha shughuli za uvuvi mdogo kwa kuzingatia masuala ya jinsia na Haki za binadamu.



1. Mwongozo wa hiari; ni nini hasa?

1.1 Mwongozo huu ni makubaliano ya aina yake, ya kwanza ya kimataifa yanayohusu uvuvi mdogo. Mwongozo unaainisha umuhimu wa uvuvi mdogo duniani, na mbinu ambazo zinaweza kutumiwa kuhakikisha kwamba uvuvi mdogo unakuwa endelevu kwa maslahi mapana ya sasa na vizazi vijavyo.

1.2 Mwongozo huu, ambao umekubaliwa na jumuiya ya kimataifa, unaainisha misingi ya kusimamia na kuendeleza uvuvi mdogo. Ni mwongozo ulioandaliwa kwa njia shirikishi, ambapo wawakilishi kutoka katika vyama mbali mbali vya wavuvi duniani, walishiriki katika hatua zote za kuuandaa chini ya uratibu wa Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO).

1.3 Mwongozo unashahidisha wale wote wanaohusika na sekta ya uvuvi mdogo, kutimiza wajibu wao kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu. Mwongozo unahimiza Serikali na Taasisi zake, jumuiya za wavuvi na wadau wengine wote kupanga na kufanya kazi kwa pamoja, ili kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu kwa manufaa ya wavuvi wadogo, watu wengine wanaojipatia riziki kutokana na uvuvi mdogo, pamoja na umma wa watu wote ambao unanufaika kwa namna mbalimbali.



2. Maudhui ya Mwongozo wa Hiari

Kuchagiza	Kuchangia	Kufanikisha
Mchango wa sekta ya uvuvi mdogo katika uhakika wa chakula na lishe, na kusaidia kuhakikisha kuna haki ya binadamu kupata chakula kinachotosheleza.	Kupatikana kwa usawa na maendeleo ya jamii ya wavuvi na kutokomeza umasikini, na hivyo kuboresha hali za kimaisha za wavuvi na wengineo katika sekta ya uvuvi kwa kuzingatia usimamizi endelevu wa rasilimali ya uvuvi.	Matumizi endelevu na usimamizi mzuri wa rasilimali ya uvuvi kama ilivyoainishwa katika miongozo mingineyo kama vile Code of Conduct for responsible Fisheries.

Kukuza	Kuainisha	Kuchagiza
Mchango wa sekta ya uvuvi mdogo kwa maslahi mapana ya baadae duniani na kwa watu wake ki uchumi, kijamii na kimazingira.	Njia zinazoweza kutumiwa na nchi mbalimbali pamoja na wadau katika kuandaa na kutekeleza sera, kwa kutumia mbinu shirikishi na kwa kuzingatia mifumo ya ikolojia, mikakati na taratibu za kisheria zitakazochagiza utumikaji wa busara na uvuvi endelevu.	Uelewa na ufahamu wa jamii yote kuhusiana na mchango mkubwa wa sekta ya uvuvi mdogo, fursa na changamoto zinazoikabili sekta huku ikizingatiwa maarifa mengi waliyonayo wavuvi wadogo ambayo yanafaa kuendelezwa.

Kwa kuzingatia misingi ya Haki za Binadamu, malengo haya ni muhimu katika kujenga uwezo wa wavuvi wadogo, ili washiriki katika michakato ya utoaji maamuzi na ili waweze kushiriki kikamilifu kuhakikisha uvuvi endelevu.

3. Takwimu za ujumla za uvuvi mdogo

Karibuwatu **milioni 120** duniani kote wamejiajiri au kuajiriwa kwa muda wote ama kama sehemu ya ajira, na hivyo maisha yao yanategemea sana shughuli zinazoambatana na mnyororo wa thamani wa sekta ya uvuvi

Zaidi ya **asilimia 90** ya wavuvi wote duniani hujishughulisha na uvuvi mdogo

Wavuvi na watu wengineo wanaofanya kazi zinazoambatana na uvuvi wapatao milioni **5.8** hupata pato dogo sana la wastani wa chini ya dola 1 ya Kimarekani kwa siku.

Asilimia 50 ya watu wote wanaofanya kazi zinazohusiana na uvuvi, ikijumuisha mnyororo wake wa thamani, ni wanawake

Asilimia 95 ya samaki na mazao mengineo ya uvuvi hutumika kwa chakula katika maeneo yanapofanyikia uvuvi husika

Asilimia 90 ya wavuvi wadogo na wale wanaojihusisha na kazi za sekta ya uvuvi mdogo wapo katika nchi zinazoendelea

4. Umuhimu wa Mwongozo huu

4.1 Umuhimu wa Mwongozo huu unatokana na ukweli kwamba; pamoja na kwamba wavuvi wadogo wanachangia asilimia kubwa ya samaki wanaovuliwa katika nchi nyingi, jamii za wavuvi wadogo zimebaki kuwa maskini, zimeachwa nyuma na kunyimwa haki wanazostahili kwa ajili ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

4.2 Hivyo, kutokana na hali hiyo, utekelezaji wa Mwongozo huu utasaidia kuleta mabadiliko chanya, ambayo yatapelekea kuchukuliwa kwa hatua zitakazofanikisha yafuatayo:

- Kuimarisha uhakika wa chakula duniani;
- Kukuza mchango wake kiuchumi na maendeleo ya kijamii;
- Kuchangia kuboresha hali ya maisha ya jamii za wavuvi hususani walioajiriwa/ kujiajiri katika sekta ya uvuvi; na
- Kufanikisha matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

4.3 Mwongozo utasaidia kuongeza uelewa wa jamii juu ya jukumu, mchango na uwezo wa wavuvi wadogo katika Sekta ya Uvuvi. Uelewa utakaopelekea jamii za wavuvi wadogo kupewa fursa na uwezo wa kushiriki, katika mchakato wa kupanga na kutoa maamuzi katika masuala mbali mbali yanayohusu usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali ya uvuvi. Yote haya yakifanyika kwa kuzingatia wajibu wa kusimamia uvuvi endelevu na misingi ya haki za binadamu.

5. Historia ya uandaaji wa Mwongozo

2008	Kongamano la kwanza la Dunia lilifanyika huko Bangkok, Thailand kujadili misingi na mbinu za kuufanya uvuvi mdogo uwe wa manufaa zaidi kwa wavuvi wadogo, na umuhimu wa kuhakikisha kazi za uvuvi mdogo zinafanyika kwa kuzingatia misingi ya Haki za binadamu. Na uamuzi ukafanyika; ni budi Mwongozo unaohusu masuala ya uvuvi mdogo uandaliwe.
2009	Kikao cha 28 cha Kamati ya Uvuvi ya FAO (Committee on Fisheries-COFI), kilichagiza na kutoa mwito wa kuwa na Mwongozo wa Kimataifa, utakaosaidia juhudi za nchi na jumuiya ya kimataifa katika kuhakikisha uvuvi mdogo unapewa msukumo na unakuwa endelevu duniani.
2010	FAO iliandaa Makongamano ya Kikanda; Afrika, Asia, Visiwa vya Pacific, na Amerika kusini pamoja na nchi za Caribbean ili kupata ushauri wa wadau, na kuainisha taratibu bora za usimamizi wa rasilimali na uvuvi mdogo. Kadhalika kupata michango juu ya namna bora za kuwasaidia wavuvi wadogo ili waweze kunufaika zaidi.
2011	Kikao cha 29 cha COFI kilipitia mapendekezo yaliyotolewa katika Makongamano ya Kikanda, na kuidhinisha kuwa Mwongozo unaohusu wavuvi wadogo uandaliwe ambao utaongezea maelekezo yaliyomo katika “Code of Conduct For Responsible Fisheries”.
2011 2012 2013	Rasimu ya kwanza ya Mwongozo wa hiari iliandaliwa kwa njia shirikishi ambapo zaidi ya wadau 4000 wakiwakilisha jamii za wavuvi, asasi za kiraia, serikali, Taasisi za kikanda kutoka nchi zaidi ya 120 walishiriki. Aidha, Asasi za kiraia zilisaidia kwa kuandaa makongamano zaidi 20 ya nchi na kikanda ili kupata maoni. Kwa upande mwingine FAO iliandaa makongamano mengine matatu ya kikanda kwa nchi za Near East, Afrika Kaskazini, Visiwa vya Pacific na Caribbean.
2013 2014	Wanachama 88 wa FAO, Asasi 4 za kimataifa zisizo za kiserikali, Taasisi 11 za kiserikali, pamoja na wawakilishi 59 kutoka Asasi za kiraia, walikutana kwa lengo la kujadiliana na hatimae kukubaliana kuhusu rasimu ya mwisho ya Mwongozo wa hiari wa uvuvi mdogo.
2014	Kikao cha 31 cha COFI kiliidhinisha Mwongozo wa hiari na kukubali mapendekezo ya FAO, kuhusu Mpango wa kusaidia utekelezaji wa Mwongozo Duniani. (Global Assistance Programme-GAP).

6. Maeneo Makuu na Mpangilio wa Mwongozo



Sehemu ya Kwanza: Utangulizi

Mwongozo huu ni wa hiari wenye wigo wa kimataifa, na unazilenga nchi zinazoendelea. Unatakiwa kutambulika na wadau katika maeneo yote ya uvuvi yakiwemo uvuvi wa bahari, maziwa, mito, na unalenga wadau wote wanaohusika na uvuvi yaani; mataifa; asasi zisizo za kiserikali za kimataifa, asasi zisizo za kiserikali za kitaifa, vyama vya kiraia, taasisi za elimu na sekta binafsi.

Mwongozo huu unatambua kuwa Sekta ya Uvuvi mdogo ina mwingiliano mkubwa wa mbinu za uvuvi na washiriki, na hivyo ni vigumu kuwa na tafsiri inayofanana kwa mataifa yote. Kwa hiyo, kwa kutumia viwango vinavyowekwa na mwongozo huu, mataifa yanashauriwa kutumia njia shirikishi ili kupata tafsiri inayokubalika ya uvuvi mdogo, na kuwatambua wale waliosahaulika na waliochwa nyuma zaidi kushirikishwa katika sekta hii. Mwongozo huu unapaswa kutafsiriwa na kutumika kwa mujibu wa mifumo ya kisheria ya kitaifa na taasisi ya nchi husika.

7. Malengo mahsusi

7.1 Mwongozo huu unaweza kutumika kwenye kufanya marekebisho na kuchochea uundaji wa sheria na kanuni mpya au za nyongeza. Hata hivyo, vipengele katika mwongozo visisomeke kama vikwazo au kudhoofisha haki au majukumu yoyote ambayo serikali inaweza kuwa nayo chini ya sheria za kimataifa.

7.2 Mwongozo huu unalenga kuongeza uelewa wa jamii juu ya jukumu, mchango na uwezo wa wavuvi wadogo katika Sekta ya Uvuvi. Malengo haya hayana budi kutimizwa kwa mtazamo unaoendeleza haki za binadamu. Msisitizo ni kwamba, jamii za wavuvi wadogo zinapaswa kupewa uwezo wa kushiriki, katika mchakato wa kutoa maamuzi, na kubeba wajibu wa kusimamia uvuvi endelevu.

8. Chimbuko na wigo

8.1 Mwongozo wa uvuvi mdogo ni matokeo ya changamoto wanazopata wavuvi wadogo hasa katika nchi zinazoendelea duniani kote. Changamoto hizo zimesababisha hali zao kuendelea kuwa duni, mbali na ukweli kwamba wao ni wazalishaji wakubwa wa chakula. Hivyo, Mwongozo unalenga kusaidia kuonyesha njia ya namna ya kusawazisha madhira hayo kwa ajili ya ustawi wa wavuvi wadogo na uvuvi endelevu kwa faida ya watu wote. Mwongozo ni wa hiari, ambao unapaswa kutafsiriwa na kutumiwa kulingana na haki na wajibu wa sheria za kitaifa na kimataifa, na kwa kuzingatia makubaliano ya hiari chini ya vyombo husika vya kikanda na kimataifa.

9. Misingi Mikuu

9.1 Mwongozo huu una misingi mikuu 13 inayoendana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, vinavyojali majukumu ya uvuvi na shughuli za maendeleo endelevu kwa kuzingatia makundi yaliyosahaulika, na kuachwa nyuma kimaendeleo pamoja na haja ya kusaidia kuendelea kutambua haki ya kupata chakula cha kutosha.

9.2 Misingi hiyo inajumuisha:

1) Haki za binadamu na utu;
2) Heshima ya mila na tamaduni;
3) Kutobaguliwa;

4) Usawa na haki za kijinsia;
5) Haki sawa kwa wote;
6) Mashauriano na ushiriki;
7) Utawala wa sheria;
8) Uwazi;
9) Uwajibikaji;
10) Uendelevu wa kiuchumi, kijamii na kimazingira;
11) Mbinu za kiujumla na jumuishi;
12) Wajibu wa kijamii; na
13) Uwezekano wa uwepo kwa uchumi mzuri wa kijamii.

10. Uhusiano na miongozo mingine

10.1 Mwongozo huu wa hiari hauna misigano yoyote na miongozo mingine iliyokubaliwa kimataifa kama vile “Code of Conduct for Responsible Fisheries” au ule Mwongozo wa Hiari kuhusu Usimamizi wa maeneo ya Uvuvi, Ardhi na Misitu. Tofauti pekee iliyopo ni kwamba, Mwongozo huu umejikita mahususi katika kuainisha kwa uwazi, na kina zaidi masuala yanayohusu uvuvi mdogo ili yaweze kueleweka na kushughulikiwa kwa urahisi na haraka zaidi.

Sehemu ya Pili: Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi Mdogo

11. Kuwajibika Katika Usimamizi na Umiliki wa Maeneo

11.1 Maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni na kuhakikisha kuwa haki za Jamii za wavuvi wadogo zinapaswa kuwa na haki kamili za kumiliki, na kusimamia rasilmali za uvuvi kwa kuzingatia usawa na utambuzi wa tamaduni zao. Hii ni pamoja na haki ya kumiliki na kusimamia maeneo ya uvuvi, ardhi na misitu iliyokaribu. Ni muhimu kwa haki hii kuzingatia haki ya wanawake. Mifumo yote ya haki itambuliwe kihalali, iwekwe kwenye kumbukumbu na kuzingatiwa.

11.2 Ufuatiliaji wa haki hizi ni muhimu upewe utambuzi wa kisheria, hususan kwa kuzingatia haki za kimila, na kutoa kipaumbele kwa wavuvi kumiliki na kusimamia rasilimali za bahari, maziwa, mito na mabwawa. Pale ambapo sheria itaainisha haki za wanawake, ni muhimu kuwa zianishwe kwenye mfumo mzima wa usimamizi.

11.3 Ni muhimu kutambua wajibu wa wavuvi wadogo na wenyeji/wazawa katika kurejesha, kuhifadhi, kulinda na kusimamia kwa pamoja ikolojia ya bahari, maziwa, mito na pwani. Katika maeneo ambayo taifa linamiliki au kudhibiti ardhi na rasilimali za bahari Maziwa na mito, haki zao za umiliki zinapaswa kuanzishwa kwa kutilia maanani malengo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira, hususani, kuzingatia matumizi na usimamizi wa pamoja kwa wavuvi wadogo.

11.4 Haki maalum kwa wavuvi wadogo kuvua katika bahari, maziwa na mito ya nchi imeingizwa katika Kanuni za Maadili ya Uvuvi Unaozingatia Uwajibikaji (Ibara 6.18) wa Shirika la Chakula na Kilimo Dunia (FAO). Kwa kuzingatia hili, ni muhimu kwa nchi kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wavuvi wadogo. Hii iwe ni kabla ya kuwekeana mikataba na makundi mengine (kwa mfano wavuvi wakubwa), ili haki na matumizi ya rasilimali za uvuvi kwa wavuvi wadogo ziheshimiwe.

11.5 Watumiaji wengine wanaongeza ushindani katika maeneo ya wavuvi wadogo, na kusababisha migogoro. Nchi zinapaswa kuhakikisha kwamba jamii za wavuvi wadogo wanapewa kinga maalum, na hawahamishwi kiholela au kwamba haki zao halali za umiliki haziingiliwi na kuondolewa. Katika suala la miradi ya maendeleo mikubwa, nchi pamoja na wahusika wengine wanapaswa kufanya mashauriano pamoja na, tathimini ya madhara yatokanayo na athari hizi kwa jamii za wavuvi wadogo.

11.6 Migogoro ya haki ya umiliki inayohusisha jamii za wavuvi wadogo ni muhimu kutatuliwa na serikali kwa wakati, gharama nafuu na ufanisi na pia iruhusu suluhisho ikiwa pamoja na kurejeshewa, kinga, fidia kila inapobidi kutekelezwa mara moja.

11.7 Majanga ya asili na migogoro ya kivita ambayo husababisha uhamisho wa lazima kwa jamii za wavuvi wadogo, yanaendelea kuathiri maisha yao sehemu nyingi. Ili kupunguza athari hizi, ni muhimu kwa nchi kuchukua kila hatua kurejeshea jamii hizi maeneo yao ya mavuvi, na maeneo ya pwani ili kuwezesha uendelevu wa uvuvi. Katika mazingira haya, mbinu za kuzifidia jamii ambazo zimeathirika vibaya na ukiukwaji wa haki za binadamu zichukuliwe pamoja na kukabiliana na ubaguzi wowote dhidi ya wanawake katika umiliki wa maeneo haya.

12. Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Uvuvi

12.1 Ni muhimu kwa hatua kuchukuliwa kwa ajili ya hifadhi ya muda mrefu na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi. Aidha, mahitaji na fursa za wavuvi wadogo zinatakiwa kutambuliwa. Haki ni lazima kuendana na wajibu. Haki ya kumiliki izingatie uwiano, uhifadhi na matumizi endelevu ya mavuvi.

12.2 Wavuvi wadogo wanapaswa kutumia mbinu endelevu za uvuvi ambazo hazina madhara kwenye mazingira na viumbe hai vya majini. Nchi zinapaswa kusaidia uvuvi mdogo kuchukua jukumu la usimamizi wa rasilimali. Vile vile, nchi zinapaswa kuhusisha jamii katika kubuni, kupanga na kutekeleza mikakati ya usimamizi, kuhakikisha ushiriki sawa wa wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi. Nchi zinapaswa kuendeleza mifumo shirikishi ya usimamizi kulingana na sheria za kitaifa.

12.3 Nchi zinapaswa kubuni mifumo ya ufuatiliaji, udhibiti na uangalizi iliyo bora na inayoendeana na uvuvi mdogo. Nchi zinapaswa kujitahidi kuepusha, kuzuia na kutokomeza mbinu zote za uvuvi zilizo haramu na haribifu; na wavuvi wadogo wanapaswa kuwezesha mifumo ya ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kushirikiana na ngazi za usimamizi katika Sekta ya Uvuvi.

12.4 Nchi zinapaswa kufafanua wajibu na majukumu ya pande zote zinazounda mfumo wa usimamizi shirikishi, kwa kufuata michakato inayokubalika kisheria. Wavuvi wadogo wawakilishwe katika vyama na vyombo husika vya kitaalamu, katika ngazi zote ili waweze kushiriki katika kufanya maamuzi na uundaji wa sera.

12.5 Katika kukuza usimamizi shirikishi, nchi pamoja na wavuvi wadogo wanapaswa kuwawezesha wanawake na wanaume, wanaoshiriki katika uvunaji na shughuli zingine katika mfumo wote wa mnyororo wa thamani wa uvuvi mdogo, ili waweze kuchangia maarifa, maoni na mahitaji yao katika sekta hii.

12.6 Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa haki ya umiliki wa Mavuvi na kutengewa maeneo maalumu ya shughuli za uvuvi kwa jamii za wavuvi wadogo, watumiao maeneo yaliyo kwenye mipaka ya maeneo ya maji na yanayoingiliana na nchi mbalimbali inalindwa. Nchi zinapaswa kuepuka hatua za kisera na kifedha zinazochangia kuzidisha viwango vya uvuvi ambavyo vitaathiri ustawi wa wavuvi wadogo.

13. Maendeleo ya Jamii, Ajira na Usalama kazini

13.1 Wahusika wote wanapaswa kuchukua mtazamo wa kiujumla juu ya maendeleo na usimamizi wa uvuvi mdogo. Nchi zinapaswa kuwekeza katika sekta za afya, elimu, kusoma na kuandika, ikiwemo digitali na ujuzi mwingine wa kiufundi katika jamii za wavuvi.

13.2 Nchi zinapaswa kukuza mipango ya hifadhi za jamii kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi mdogo, na wadau wake wote katika mnyororo wa kuongeza thamani kwa mazao ya uvuvi. Nchi zinapaswa kuendeleza miradi kwa ajili ya kuweka akiba, mikopo na bima, pamoja na msisitizo juu ya ushirikishwaji na upatikanaji wa huduma hizi kwa wanawake.

13.3 Wahusika wote wanapaswa kutambua kuwa shughuli mbalimbali katika mnyororo wa kuongeza thamani kwa mazao ya uvuvi, yatokanayo na uvuvi mdogo kuwa ni shughuli za kiuchumi na kitaaluma.

13.4 Pia, nchi zinapaswa kuzingatia ajira zenye staha. Nchi zinapaswa kuhakikisha kuwa haki za wavuvi na wafanyakazi katika sekta ya uvuvi, zinatambuliwa hadi wanapofikia kiwango kizuri cha ubora wa maisha. Nchi zinapaswa kufuata njia zisizo za ubaguzi na sera bora za kiuchumi, ili wafanyakazi hawa wapate mapato yanayowiana na kazi zao, mitaji na usimamizi wao.

13.5 Nchi na wahusika wengine wanapaswa kusaidia fursa mbadala za kukuza mapato. Mazingira sahihi yanapaswa kuandaliwa kwa ajili ya jamii za wavuvi wadogo kufanya shughuli zinazohusiana na uvuvi. Uhamaji ni mkakati wa kawaida wa kujikimu kimaisha. Nchi zinapaswa kutambua na kushughulikia visababishi na madhara ya mienendo ya wavuvi wanaohamahama kati ya mipaka ya nchi jirani.

13.6 Nchi zinapasa kushughulikia afya, usalama na mazingira ya kazi yasiyoridhisha. Nchi pia zinapaswa kuzuia ajira za kulazimishwa na utumwa unaotokana na madeni. Nchi zinapaswa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za shule na vifaa vya elimu, kutambua umuhimu wa ustawi na elimu ya watoto kwa maisha yao ya baadaye. Umhimu wa hali ya usalama katika bahari, maziwa na mito na sababu mbalimbali zinazotekeleza hali hii zinapaswa kutambuliwa na wahusika wote. Ni muhimu kujua, usalama na uhakika wa afya kazini kwa wavuvi wadogo, vinajumuishwa katika utaratibu mzima wa usimamizi wa uvuvi. Nchi zinapaswa kulinda haki za binadamu na utu wa wadau wa uvuvi mdogo katika nyakati za migogoro ya vita.

14. Mnyororo wa Thamani, Uhifadhi na Biashara

14.1 Jukumu kuu la wavuvi wadogo katika Sekta ya Uvuvi linapaswa litambulike na wadau wote. Aidha, wanawake wanatakiwa kushiriki na kupewa nafasi kubwa katika Sekta ya Uvuvi, kwa kuwa asilimia kubwa wanajihusiha baada ya samaki kuvuliwa, hili pia linapaswa kutambulika na wadau wote. Ni muhimu kwa serikali kuwekeza katika miundo mbinu sahihi, miundo ya kitaasisi na kujenga uwezo wa wavuvi katika hatua zote zinazohusu uvuvi mdogo. Mifumo ya asili ya ushirikiano kati ya wavuvi na wanaofanya shughuli za uvuvi itambuliwe kihalali.

14.2 Ni muhimu kubuni mbinu za kuepusha hasara kwenye uzalishaji katika mfumo mzima wa mnyororo wa uongezaji thamani katika uvuvi. Nchi zinapaswa kukuza biashara yenye usawa na isiyo ya kibaguzi, ya bidhaa za wavuvi wadogo katika masoko ya ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa. Lakini, ni muhimu kuwa makini katika uendelezaji wa biashara ya kimataifa ya mazao ya uvuvi, ili isiathiri mahitaji ya lishe ya jamii zinazotegemea samaki kwa ustawi wake kiujumla.

14.3 Faida kutokana na biashara ya kimataifa inapaswa kugawanywa kwa usawa na mifumo ya usimamizi wa uvuvi inapaswa kuwekwa, ili kuzuia uvunaji wa rasilimali za uvuvi usio endelevu na unaosukumwa na mahitaji ya soko. Ni muhimu kwa tathmini za kimazingira, kijamii na kiuchumi ziwe ni sehemu ya sera na taratibu zinazochukuliwa, ili kuhakikisha kwamba athari zitokanazo na biashara ya kimataifa juu ya mazingira na utamaduni, uhakika wa chakula na maisha ya wavuvi wadogo yanaweza kupimwa na kushughulikiwa kwa usawa. Serikali iwezeshe upatikanaji wa taarifa za masoko, na biashara kwa wakati na zilizo sahihi kwa wadau katika mfumo wa mnyororo wa kuongeza thamani wa wavuvi.

15. Usawa wa Jinsia

15.1 Mikakati ya uendelezaji uvuvi mdogo inapaswa ianishe masuala ya haki za kijinsia. Nchi zinapaswa kuzingatia wajibu wao chini ya sheria za kimataifa za haki za binadamu na kutekeleza makubaliano ambayo nchi wanachama wameafikiana yanayohusiana na masuala ya wanawake. Hatua maalum za kushughulikia ubaguzi wa wanawake zichukuliwe. Usawa wa kijinsia ni muhimu ufikiwe kwa kuunda sera na sheria na kubadilisha zile ambazo hazilingani na lengo hili. Mifumo ya tathmini iendelezwe ili kuangalia matokeo ya sheria, sera na mikakati inayochukuliwa kuboresha hadhi ya wanawake na kupata usawa wa kijinsia. Teknolojia bora na zilizo sahihi kwa shughuli za wanawake zinapaswa kuendelezwa.

16. Hatari za Majanga na Mabadiliko ya Tabia Nchi

16.1 Kupambana na mabadiliko ya tabia nchi kunahitaji hatua za haraka na zenye ubunifu, na tahadhari maalumu inapaswa kuzingatiwa kwa ajili ya jamii ya wavuvi wadogo wanaoishi katika visiwa vidogo. Mbinu shirikishi kwa kushirikiana na sekta mtambuka zinahitajika. Ni muhimu kwa mbinu za kukabiliana na majanga pamoja na misaada iwe inatolewa pale inapohitajika.

16.2 Wahusika wote wanaosababisha majanga yanayoathiri shughuli za uvuvi mdogo wanapaswa kuwajibishwa. Athari za mabadiliko ya tabia nchi na majanga katika uvuvi na masoko zinapaswa kuzingatiwa. Dhana ya “kuongeza ubora zaidi’ inapaswa kutumika katika kukabiliana na maafa. Aidha, ni muhimu kuhimiza na kukuza matumizi ya nishati endelevu katika mfumo mzima wa uongezaji thamani wa mazao ya uvuvi

17. Sehemu ya Tatu: Kujenga Mazingira Bora na Kusaidia Utekelezaji wa Mwongozo

17.1 Kujenga mazingira bora na kusaidia utekekelezaji wa Mwongozo

- Kuimarisha uhusiano na mashirikiano ya kisera baina ya taasisi mbalimbali
- Kufanya tafiti na upashanaji wa taarifa za usimamizi wa raslimali ya uvuvi
- Kujenga uwezo wa wadau na Taasisi
- Kusaidia utekelezaji, ushirikiano na ufuatiliaji

18. Kuimarisha uhusiano na mashirikiano ya kisera baina ya taasisi mbalimbali

18.1 Ili kukuza maendeleo ya kiujumla katika jamii za wavuvi wadogo, nchi zinapaswa kutambua umhimu wa sera zinazowiana na kujitahidi kuimarisha uwiano huo, baina ya sera za nchi na sera za kimataifa zinazosimamia haki za binadamu na utu; pamoja na sera mtambuka zinazohusiana na maendeleo ya jamii; elimu; afya; kazi na ajira; Biashara; utunzaji na usimamizi wa mazingira; kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi; na kuimarisha uwekezaji katika jamii za wavuvi wadogo. Utekelezaji wa sera utazingatia usawa na haki za kijinsia.

18.2 Nchi zinapaswa kutengeneza na kutumia mbinu za upangaji wa matumizi ya maeneo kwa kuzingatia maslahi ya wavuvi wadogo, na majukumu yao katika usimamizi unaojumuisha maeneo ya Ukanda wa Pwani, Maziwa na Mito. Nchi zinapaswa kuchukua hatua za kisera ili kuainisha na kuoanisha mifumo na sera zinazoathiri uhai wa ikolojia ya bahari, mito na maziwa.

18.3 Sera ya uvuvi inapaswa kutoa dira ya muda mrefu kwa ajili ya uvuvi mdogo ulio endelevu. Ni muhimu kuainisha maeneo maalumu ya mawasiliano katika mamlaka za serikali na mashirika kwa ajili ya jamii za wavuvi wadogo. Wadau wa uvuvi mdogo wanapaswa kukuza ushirikiano miongoni mwa vikundi/mashirika yao. Nchi zinapaswa kukuza mifumo ya utawala bora inayochangia usimamizi madhubuti wa uvuvi mdogo. Ushirikiano wa kimataifa na kikanda unahitajika ili kuwa na uvuvi endelevu.

18.4 Kuimarisha mashirikiano baina ya wadau wa uavuvi mdogo, taaisisi zao, na asasi za kiraia na zisizo za kiraia, ili kuunda jukwaa la kupashana taarifa, kujenga uelewa na kubadilishana uzoefu, pamoja na kuboresha ushiriki wao katika maamuzi na utekelezaji wa sera kwenye jamii za wavuvi wadogo.

18.5 Nchi inatakiwa kutambua na kuimarisha Mfumo wa halmashauri za wilaya na serikali za mitaa ili kuboresha usimamizi endelevu wa raslimali ya uvuvi kwa kuzingatia usimamizi wa uvuvi mdogo unaojumuisha ikolojia na mazingira.

19. Kufanya Tafiti na Upashanaji wa Taarifa za Usimamizi wa Raslimali ya Uvuvi

19.1 Nchi zinapaswa kuanzisha na kuimarisha katika hali ya uwazi, mifumo sahihi ya ukusanyaji wa takwimu za uvuvi, ambazo ni takwimu za: uzalishaji wa samaki; uuzaji na ununuaji wa samaki na mazao yake ndani na nje ya nchi; ulaji wa samaki; kiuchumi na kijamii kuhusiana na uvuvi; ikolojia; uwingi wa samaki waliopo majini; na kibaiologia, kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi kwa wakati kuhusiana na usimamizi endelevu wa uvuvi mdogo.

19.2 Ufanisi wa maamuzi unahitaji mawasiliano ya taarifa sahihi. Nchi zinapaswa kujitahidi kuzuia rushwa, kuongeza uwazi na kuhakikisha watoa maamuzi wanawajibika.

19.3 Jamii ya wavuvi wadogo wanapaswa kuwa wapokeaji, wamiliki na watoaji wa elimu. Taarifa ambazo ni za muhimu kwa ajili ya uvuvi mdogo unaowajibika, pamoja na maendeleo endelevu, zinapaswa kutolewa. Maarifa, utamaduni, desturi na teknolojia za jamii za wavuvi wadogo zinapaswa kutambuliwa na kuwekwa kwenye kumbukumbu.

19.4 Nchi zinapaswa kuunga mkono jamii za wavuvi wadogo hususan wazawa na wanawake wanaotegemea uvuvi kwa ajili ya kujikimu. Ni muhimu vilevile, kuwa na mifumo sahihi na mitandao iliyopo katika ngazi ya jamii, ngazi ya kitaifa na ngazi za juu itumike kukuza ubadilishanaji na upashanaji wa taarifa katika sekta ya uvuvi.

19.5 Nchi zinapaswa kutenga fedha kwa ajili ya utafiti wa uvuvi mdogo na kuhimiza ukusanyaji shirikishi wa takwimu na tathmini ya sekta hii.

19.6 Nchi zinapaswa kuendeleza utafiti katika maeneo mbalimbali hasa katika muktadha wa mahusiano ya kijinsia, ili kuelekeza mikakati ambayo itahakikisha usawa wa manufaa yatokanayo na mikakati hii kwa wanaume na wanawake katika uvuvi.

19.7 Nchi zinapaswa kuendeleza matumizi ya samaki katika mipango ya elimu kwa walaji, ili kupanua ufahamu wa jukumu la wavuvi na uvuvi mdogo, na ili kuongeza ufahamu wa faida za kiafya za kula samaki.

20. Kujenga Uwezo wa Wadau na Taasisi

20.1 Uwezo wa kushiriki katika mchakato wa kutoa maamuzi uimarishwe. Nchi zinapaswa kujenga uwezo kwa wavuvi wadogo ili waweze kunufaika na fursa za masoko zilizopo. Mifumo ya kujenga uwezo inaweza kuwa ni ya aina mbili; kwanza ni kuendeleza kujenga uwezo juu ya maarifa na ujuzi ili kuwezesha maendeleo endelevu; na pili- ni muhimu kuwa na mipango ya usimamizi shirikishi inayofanikiwa.

20.2 Wadau wote wanatakiwa kutekeleza Mwongozo huu wa wavuvi wadogo ili kuwa na uvuvi endelevu. Umoja wa Mataifa na Mashirika yake mahsusi yanapaswa kuunga mkono juhudi za nchi katika kutekeleza Mwongozo huu. Nchi na washirika wengine wanapaswa kushirikiana katika kujenga uelewa wa Mwongozo huu, na kuusambaza kwa walengwa.

21. Kusaidia utekelezaji, ushirikiano na ufuatiliaji

21.1 Umuhimu wa mifumo ya ufuatiliaji unapaswa kutambuliwa. Wawakilishi halali wa jamii za wavuvi wadogo wanapaswa kushirikishwa katika, uendelezaji na utekelezaji wa mikakati ya Mwongozo huu na katika ufuatiliaji wake. Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), linapaswa kukuza na kusaidia katika mipango ya maendeleo ya kidunia.

21.2 Nakala nzima ya Mwongozo huu wa hiari kwa ajili ya kuhakikisha uvuvi mdogo ulio endelevu katika muktadha wa uhakika wa chakula na kuondoa umaskini unapatikana katika tovuti: http://www.fao.org/documents/card/en/c/I4356SW

Mwongozo wa hiari wa kuhakikisha uvuvi mdogo unakuwa endelevu; katika muktadha wa uhakika wa chakula na kuondoa umaskini umeandaliwa kama nyongeza ya Taratibu za Kimaadili za Uvuvi zinazozingatia uwajibikaji, ambazo ziliandaliwa chini ya uratibu wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) mwaka 1995 (Code of Conduct for Responsible Fisheries CCFRF) na kukubaliwa nchi nyingi duniani. Aidha, Mwongozo huu wa hiari ni mahsusi kwa ajili ya kuangaza na kuweka taratibu zinazuhusu uvuvi mdogo. Sababu kuu iliyopelekea kuandaa Mwongozo maalumu kwa ajili ya uvuvi mdogo ni kwamba; kwa kiwango kikubwa jamii ya wavuvi wadogo imeendelea kuachwa nyuma, na umaskini katika jamii hizi umekuwa ni wa kiwango kikubwa. Hali hii ya kusikitisha inatokea wakati ambapo uvuvi mdogo huchangia nusu ya samaki wote wanaovuliwa duniani, na huajiri asilimia 90 ya wavuvi na wafanyakazi wengine katika Sekta ya Uvuvi duniani. Hivyo, imeonekana kuna umuhimu mkubwa wa kuandaa Mwongozo huu, ili kuangazia changamoto mbalimbali zinazowakabili wavuvi wadogo, na kubainisha mbinu ambazo zinaweza kutumiwa katika kutatua changamoto hizo. Mwongozo unabainisha masuala yote muhimu katika mfumo mzima wa mnyororo wa thamani ikiwa ni pamoja na usimamizi wa rasilimali ya uvuvi, masuala ya maendeleo ya jamii ya wavuvi wadogo, thamani ya mazao na biashara, pamoja na umuhimu wa kujenga mazingira bora yanayoimarisha shughuli za uvuvi mdogo kwa kuzingatia masuala ya jinsia na Haki za binadamu.

I4356SW/1/02.19